



EAST AFRICAN COMMUNITY

TAARIFA YA AWALI YA MKUU WA TIMU YA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA 2020 KUTOKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

1. Nilipewa heshima ya kuongoza Timu ya Watazamaji wa Uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Timu) katika Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa Mwaka 2020. Timu iliwasili hapa nchini tarehe 21 Oktoba, 2020. Timu hii inaundwa na Watazamaji 59 ambao walisambazwa katika mikoa 13 hapa nchini. Watazamaji hao, tarehe 26 na 27 Oktoba, 2020 waliweza kuangalia maandalizi ya Uchaguzi na tarehe 28 Oktoba, 2020 walitekeleza jukumu la utazamaji. Timu pia ilifuatilia utangazaji wa matokeo ya awali ya uchaguzi yaliyokuwa yanatolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na yale yaliyotolewa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar.
2. Timu ya Waangalizi ilitembelea jumla ya vituo vya kupigia kura 160. Timu ilibaini yafuatayo:-
 - a) Kwa kiwango kikubwa zoezi la uchaguzi lilifanyika katika mazingira ya Amani na Utulivu;
 - b) Vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi pamoja na wagombea wao waliendesha kampeni zao nchi nzima katika mazingira ya Amani na utulivu;
 - c) Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa kulingana na matakwa ya sheria na kanuni zinazosimamia uchaguzi;
 - d) Zoezi la upigaji kura liliendeshwa kwa uhuru, Amani na utulivu;

- e) Uchaguzi uliandaliwa na kusimamiwa kwa weledi wa hali ya juu. Timu inaipongeza tume kwa namna inavyoendelea kutoa matokeo kwa haraka kadri inavyoyapokea;
3. Katika maeneo ambayo timu iliendesha zoezi la utazamaji, imeridhika na namna zoezi la uchaguzi lilivyoendeshwa. Timu inasubiria matokeo ya Mwisho yatakayotolewa na Tume ya Uchaguzi;
 4. Timu imepokea taarifa kuwa baadhi ya viongozi wa vyama vya Siasa vilivyoshiriki uchaguzi wameelezea kutoridhishwa na namna zoezi la uchaguzi lilivyoendeshwa na mwenendo wa matokeo yanayotolewa na Tume ya Uchaguzi ya Taifa. Timu inawashauri kuhakikisha kuwa wanayasiluisa malalamiko yao kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Nchi na Sheria zinazosimamia uchaguzi nchini Tanzania. Timu inawaomba kuweka mbele maslahi ya watanzania hususan kuepuka vitendo vyovyote vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa Amani na utulivu;
 5. Kulingana na Vigezo vya Uchaguzi viliyoainishwa katika Mwongozo wa Uchaguzi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, uchaguzi huu umekidhi vigezo vyote na ulikua huru na haki;
 6. Timu ya Watazamaji kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki inachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Tanzania kwa busara waliyoionesha katika mchakato mzima wa uchaguzi hususan katika kuhakikisha wanadumisha amani na utulivu jambo ambalo ni muhimu katika mchakato huu. Timu inawasihi wananchi wa Tanzania, Wagombea nafasi ya Urais, ubunge na udiwani kukamilisha hatua zilizobaki za uchaguzi kwa Amani na utulivu;
 7. Tamko la Timu ya Watazamaji kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki litatolewa saa nane Mchana katika Hoteli ya Four Points New Afrika.

Dar es Salaam

30 Oktoba, 2020

HE Sylvestre NTIBANTUNGANYA

Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Burundi na

Kiongozi wa Timu ya Waangalizi wa Jumuiya